
# KITABU CHA MWONGOZO

# KWA

# WAALIMU WA BIBLIA

Na Jo Scales



Picha Zimechorwa na Cathy Schellenberg

# KITABU CHA MWONGOZO
# Kwa
# WAALIMU WA BIBLIA

**Kimeandikwa na JO SCALES**

**Picha zilizomo ndani zimechorwa na**
**CATHY SCHELLENBERG**

©

Copyright, 1984
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

# YALIYOMO

UTANGULIZI

1. KWA NINI? .................................... 7
2. MAFUNDISHO NI NINI? .................... 11
3. NI NANI ANAYEHITAJI KUFUNDISHWA? .......................... 21
4. MAHALI PA KUFUNDISHIA .............. 25
5. KWA NJIA GANI? .......................... 29
6. MISAADA YA MAFUNZO ................. 34
7. NJIA ZA KUFUNDISHA .................... 42
8. SASA FUNDISHA .......................... 63

# UTANGULIZI

Ulikuwa usiku wa manane. Mchungaji hakuweza kupata usingizi. Akilini mwake alifikiria juu ya maswali yaliyomtatiza mshiriki wake. Mwanawe mshiriki yule aliiba vitabu shuleni mwao. Mwalimu mkuu alimfukuza na alikataa kumrudishia karo. Huko nyumbani, babaye mwana huyo alimpiga kwa hasira. Lakini maswali ya mzazi yule kusema; "Kwa nini mwanangu aliiba? Hakujua kwamba kuiba ni kosa?" yalikuwa lazima kujibiwa. Je, ni nani aliyekosa kumfundisha mwanawe vyema? Je, ni yeye kama baba au ni kanisa?

Katika hali ya giza, mchungaji aliketi na kumwomba Mungu, akisema, "Ni kwa sababu gani jambo hili lilifanyika?' "Ni nani ambaye hakumfunza mwana huyu vizuri?" Usiku ule wa manane, jibu lilipatikana kutoka kwa Mungu. Ni wazazi ndio walioshindwa kumfundisha mwana huyo kwamba kuiba ni dhambi. Mchungaji pia hakutimiza wajibu wake. Hakuutimiza kwa sababu hakuruhusu kanisa kuwa na madarasa ya mafunzo ya Biblia. Kanisa pia lilishindwa. Halikuwa na mipango ya vijana wala nafasi kwa watu wazima kujifunza Biblia. Kulikuwa na ibada tu ya kila wiki. Ni kweli kwamba mchungaji alihubiri kila Jumapili. Mwana huyo na jamaa yake walikuwapo kila mara wakati wa mahubiri, lakini hiyo peke yake haikutosha. Jamaa ile walihitaji kufunzwa Biblia kwa ukamilifu.

Mchungaji yule alifikiria muda mwingi ambao mke wake aliutumia kumfundisha binti yao kupika. Kwanza, binti yao alikaa akimtazama mama yake jinsi alivyopika. Kisha alianza kumsaidia katika upishi. Hatua kwa hatua,

mamaye alimwongezea wajibu wa kujifunza kupika mpaka wakati alipoweza kupika vizuri (kama mamaye).

Sasa mchungaji aliwaza, "Nawezaje basi kuwatazamia watu wa kanisa langu kujifunza njia ya Mungu na mambo ya kiroho ikiwa ninawahubiria tu dakika arobaini kila juma?" Hivyo basi, mchungaji alipata ufahamu mpya mbele zake Mungu kuhusu wajibu wake kuongoza kanisa lake kuwa na mipango ya mafunzo ya Biblia kwa watu wote.

Ikiwa Mungu amekwisha kukuongoza kama alivyomwongoza mchungaji yule, kitabu hiki kitakuonyesha jinsi ya kuwa mwalimu wa mafunzo ya Biblia kanisani mwako. Mafunzo haya yanaweza kuitwa mipango ya vijana, uanafunzi, T.E.E., Umoja wa kina mama au Shule ya Jumapili.

# 1 KWA NINI?

Kuna sababu tatu zinazowapasa Wakristo kuwa na mafunzo ya Biblia na ya kiroho makanisani mwao. Sababu hizo ni:

1. Mungu huwaamuru Wakristo kuwafunza wengine.
2. Makanisa yatakua kiroho na idadi ya washiriki itaongezeka.
3. Wakristo wengi hawajafunzwa kamwe na ni wadhaifu katika imani zao, ingawa wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu.

Tutachunguza kila mojawapo ya sababu hizi.

## MUNGU HUTUAMURU TUFUNDISHE

Biblia ni dhahiri au wazi kuhusu wajibu wa Mkristo kufundisha. Neno la mwisho ambalo Yesu aliwaambia wanafunzi wake kabla ya yeye kupaa mbinguni lilikuwa kufundisha. "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:19-20).

Je, Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kufanya nini? Kufundisha! Amri hii ni yetu sisi hata leo kama vile ilivyokuwa kwa wanafunzi wake Yesu. Ni lazima tufundishe. Tukikosa kufundisha, tumetenda dhambi.

Paulo alijua ya kwamba Yesu alituachia amri kuwafundisha wengine kwa sababu alisema: "Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu, aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha

njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa" (1 Wakorintho 4:17).

Paulo, ambaye alikuwa mshonaji hema, alifuata amri ya Yesu kufundisha. Ingawa alikuwa amejifunza maarifa mengi kutoka kwa waalimu wakuu, alikuwa bado hajafunzwa jinsi ya kufundisha. Lakini aliendelea kufuata amri ya Yesu. "Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa ya Yesu. "Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwana kwa watu wote, awezaye kufundisha...." (II Timotheo 2:24). "Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uyakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine" (II Timotheo 2:2).

Petro na wanafunzi wengine walimtii Yesu. "Nao waliposikia wakaenda alfajiri hekaluni, wakaanza kufundisha" (Matendo ya Mitume 5:21).

Lakini, haya siyo maneno yote kuhusu kufundisha katika Biblia. Yesu mwenyewe alikuwa mwalimu na mfano wetu. Alipotuamuru kufundisha, alikuwa akitwambia mambo yale aliyoyatenda mwenyewe.

## MAKANISA YATAKUA

Wakristo makanisani wakifunzwa, makanisa hayana budi kukua. Hii ni rahisi kuelewa. Mungu hutubariki tunapofuata amri zake. Baraka hizi twaziona katika nguvu za washiriki wetu. Wakristo wajifunze mengi kuhusu mambo Mungu anayotazamia maishani mwao. Kufanya hivyo kunawatia moyo kumfuata Mungu katika kuwashuhudia wengine na kuwakaribisha kanisani.

Hivi ndivyo hutokea. Mtu anapowasha taa gizani, nuru chache itaonekana nje. Walakini atumiapo taa yake kuwashia nyingine, nuru huongezeka nyumbani. Aendeleapo kuwasha taa, nuru huendelea kuongezeka

nyumbani. Hatimaye nyumba hujaa nuru zaidi hata jirani huja kuona ni nini kinachoendelea nyumbani humo.

Mkristo akiwa na ujuzi na kushirikisha ujuzi huo kwa wengine nuru huongezeka kanisani. Watu hawa wawili nao wakishirikisha "nuru" hii yao, kanisa litajaa nuru hiyo kwa wingi. Jirani watakuja mbio kuona ni nini kinachoendelea kanisani.

## IMANI YA KILA MKRISTO ITAONGEZEKA

Wakristo wengi wana ujuzi mdogo sana juu ya Mungu au amri zake. Wanajua hatua chache sana za kiroho. Hawaelewi kusudi la kanisa. Wanakosa furaha tele ya Mungu na baraka kwa sababu hawamjui vyema.

Mtu ampokeapo Kristo kuwa Mwokozi wake, huwa kama mtoto mchanga aliyezaliwa. Humbidi kujifunza na kukua. Huhitaji kujifunza masomo rahisi kwanza. Biblia inasema masomo haya rahisi ni "maziwa" ya Neno la Mungu. Ni muhimu kwa Mkristo mchanga kujifunza Wakristo wengi hawapokei mafundisho ya kutosha kuwaendeleza kwa masomo magumu. "Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya" (Waebrania 5:12-14).

Hakuna mama atakayekosa kumpa mtoto mchanga maziwa ya kutosha kukua. Lakini Wakristo waliopevuka katika makanisa mengine wanakosa kuwafundisha Wakristo wao wapya ili wakue katika Kristo.

Mtoto mchanga anaweza kuongozwa kwa urahisi kufanya mambo mengi. Vivyo hivyo, Mkristo mchanga anaweza kuongozwa kwa urahisi. Anaweza kuongozwa mbali na kanisa. Au anaweza kuongozwa kuimarika, kukua na kuwa tayari kuwafundisha wengine.

Kwa nini inatupasa kufundisha makanisani? Twafundisha kwa sababu Yesu anatwamuru kufanya hivyo. Twafundisha kwa sababu twataka makanisa yetu kukua. Twafundisha kujiimarisha katika mambo ya kiroho.

# 2 MAFUNDISHO NI NINI?

Waalimu wengine hawaelewi maana ya mafundisho. Unaweza kuwasikia wazi ukiwa ndani ya darasa lingine mbali kidogo. Watu hawa wamemsikia mchungaji akihubiri kila Jumapili. Wanafikiri ati wanapaswa kufundisha jinsi mchungaji wao anavyohubiri. Wanasimama mbele ya kundi lao na kutupatupa mikono yao. Wao tu ndio wanazungumza. Wanatumia sauti za juu. Hawafundishi; bali wanahubiri. Lakini, iko tofauti.

Waalimu wengine hufikiri ati kufundisha ni kusoma na kuliongoza darasa kuimba nyimbo. Wanafunzi hawapati nafasi hata kidogo kushiriki kikamilifu katika kujifunza. Wao ni kama watazamaji tu. Ni mafundisho na masomo machache sana yanayoendelea.

Waalimu wengine nao hufikiri ati ni lazima kufurahisha washiriki wa darasa lao. Huepuka kufundisha juu ya dhambi na matokeo yake. Wanaweza kuleta peremende. Hawataki kukosea darasa lao kwa njia yo yote. Labda wanafunzi wao wanakuja darasani kufurahishwa tu wala siyo kufunzwa.

Basi, je, mafundisho ni nini? Kuna maelezo mengi sana ya mafundisho. Hii ni mojawapo. Mafundisho ni kitendo cha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Mawasiliano kutoka kwa mwalimu yatafanya maisha ya mwanafunzi kuwa ya maana sana. Sisi hufunza kanisani na katika Shule ya Jumapili ili watu wamjue Mungu vyema zaidi. Tukifundisha kweli, maisha ya wanafunzi hayana budi kubadilika.

Mafundisho mema hufuata msingi wa taratibu fulani za elimu. Taratibu hizi ni:

a) Jitayarishe vyema na kwa uangalifu.

b) Tumia milango tofauti kama inavyowezekana.

c) Heshimu wanafunzi.

d) Tumia mitindo ya mafundisho mbalimbali na vifaa tofauti.

## UTARATIBU WA KWANZA: JITAYARISHE VYEMA

Wajibu wa kufunza Biblia ni mkuu. Tunaamriwa tufundishe, walakini, tunaonywa ya kwamba mwalimu atajibu mbele zake Mungu kuhusu mafundisho yake. Ni kazi kubwa na ya kuogopesha. Basi tutaitendaje kazi hiyo? Sisi wenyewe hatuwezi, lakini Roho Mtakatifu anaweza kututumia kuifanya. Yesu aliahidi ya kwamba Mfariji atakapokuja, atatukumbusha mambo yote Yesu aliyotufundisha. Mfariji huyo ndiye mwalimu wetu.

Kazi yetu ni kukaa macho kiroho na tayari kwa mafundisho ya Roho. Tunawezaje kufanya hivyo? Kwa kujifunza Biblia na maombi. Mwalimu wa Biblia hawezi kuacha hata siku moja kupita bila kusoma Neno la Mungu. Kuna mipango mingi sana ya kutumia katika kujifunza Biblia, kama kujifunza kila mlango, kila kifungu, au kila somo. Mtindo wa kujifunza siyo muhimu, lakini jambo muhimu ni mambo tunayoyafanya.

Hapa kuna hadithi fupi itakayosaidia kuonyesha jinsi utaratibu huo unaweza kufaulu. Hapo kale palikuwa na mwuzaji vitabu aliyesafiri hapa na pale kuuza vitabu. Hakujua mengi juu ya biashara. Alipouza kitabu kimoja, alitumia pesa kwa chakula na malazi. Aliendelea vivyo hivyo, kila mara alipouza kitabu kimoja, aliendelea kubaki na vichache. Siku moja alipochungulia mkoba alioubebea vitabu, aliona kwamba alikuwa ameviuza vyote. Alitia

mkono mfukoni mwake, akaona kwamba hana pesa. Sasa hakuweza kununua vitabu vingine vya kuuza. Mtu huyu mpumbavu aligundua kwamba ilimpasa kununua vitabu vingine kuchukua mahali pa vile alivyouza ili biashara yake iendelee.

Baadhi ya waalimu wengine wa Biblia wanaweza kushindwa katika njia sawa na hiyo. Huendelea kufundisha mambo ya kiroho bila kumwendea Mungu kupewa ujuzi mpya. Njia ya pekee kujua kwamba una jambo la kufundisha ni kwa maombi na mafunzo ya Biblia.

## UTARATIBU WA PILI: TUMIA MILANGO TOFAUTI WAKATI WA KUFUNDISHA.

Mwili una milango au njia tano za maarifa ambayo ni ya mawasiliano. Milango hii ni macho, masikio, pua, midomo na akili ya kupapasa. Mawasiliano yetu yote hupitia milango hii. Majaribu yameonyesha kwamba ikiwa zaidi ya mojawapo ya milango hii ikitumiwa katika kufundisha, basi mafunzo mengi hupatikana. Kutokana na mahubiri ya mchungaji tunaweza kukumbuka mambo muhimu na hadithi anayosimulia. Lakini baada ya siku mbili au tatu tunasahau baadhi ya mambo tuliyokumbuka. Juma moja baadaye, tutaweza kukumbuka mambo machache. Baada ya mwezi, pengine hatutaweza kamwe kukumbuka mahubiri yale. (Mara kwa mara sisi husahau mengi tunayoyasikia pasipo milango mingine yametumiwa.)

Kwa mfano, mwalimu anaweza taka kufundisha jinsi kijiji fulani kilionekana wakati wa Yesu. Atasimulia juu ya kijiji kile kwa maneno. Mwanafunzi atatumia masikio yake kama mlango wa kupokea mawasiliano hayo. Baadaye mengi ya mawasiliano hayo aliyosikia husahaulika. Mwalimu mwingine anayepanga kufundisha somo lile lile

anaamua kueleza jinsi kijiji kile kilionekana, lakini anaonyesha picha za kijiji kile. Mwalimu huyu atakuwa ametumia milango miwili ya mawasiliano: masikio na macho. Ameimarisha maneno yake kwa picha. Baadaye mwanafunzi atakumbuka zaidi jinsi kijiji kile kilionekana.

Sisi hupokea mawasiliano mengi kwa njia ya kuonja na kunusa. Lakini njia hizi si muhimu zaidi katika mafunzo ya Biblia kuliko zile nyingine tatu.

Mwalimu anayefaulu katika mafunzo yake hukumbuka kwamba kusudi lake kufundisha ni kubadili maisha. Akitaka mafunzo yake yalete mabadiliko anayotaka, ni lazima kutumia milango mingi ya mawasiliano kama anavyoweza.

**UTARATIBU WA TATU: HESHIMU WANAFUNZI WAKO.**

Mara kwa mara twasikia, "Mwalimu huyu ni mzuri," au "Mama huyu ndiye mwalimu bora sana ambaye amewahi kunifundisha." Je, ni kitu gani kinachomfanya mwalimu kuwa mzuri au bora? Kwa nini sisi husema ati mwalimu fulani ni bora zaidi kuliko mwingine? Mwalimu mzuri ni yule anayejali wanafunzi wake. Anawaheshimu. Mwalimu anaweza kuonyesha heshima hii kwa wanafunzi wake katika njia tano tofauti. Njia hizo ni:

a. Kuwa na darasa la wanafunzi wachache. Darasa linapaswa kuwa na wanafunzi kumi hadi kumi na wawili. Washiriki wa darasa lako wanapofika tisa, uanze kumtafuta mwalimu mwingine kuchukua nusu ya darasa. Baada ya mgawanyiko kufanywa, -- utaona ajabu jinsi kila nusu ya darasa hilo lililogawanywa linaweza kukua!


Darasa likiwa na wanafunzi wachache, mwalimu atamjua kila mshiriki vizuri. Mwalimu asiyeelewa udhaifu, uhusiano na mahitaji ya darasa lake, hawezi kuwafundisha vyema.

b. Kuwatembelea wanafunzi kwa mpango. Maana yake kwamba kila mwalimu anastahili kujua wakati wa mwisho alipomtembelea mwanafunzi. Apange kumtembelea mwanafunzi ikiwezekana mara moja kwa mwezi nyumbani kwao. Hii ni sababu nyingine ya kulifanya darasa kuwa na wanafunzi wachache. Mwalimu hawezi kuwatembelea washiriki wake wakiwa 30 au 40 darasani.

Tukitaka hasa kuwafahamu wanafunzi wetu, hatuna budi kuwatembelea nyumbani mwao. Iwapo tuna mtu darasani mwetu ambaye haleti jamaa yake kanisani, tunaweza kumwelewa vyema tukimtembelea nyumbani. Mwanafunzi anaweza kuwa wazi sana na mwalimu wake kwa kushiriki naye shida na mahitaji yake.

Mwanafunzi akitembelewa na mwalimu nyumbani kwao, atatambua kwamba mwalimu anamjali. Ataona ya kwamba yeye ni muhimu kwa mwalimu wake.

Matembezi yako yawe mafupi. Mwanafunzi aongee kadiri anavyotaka. Tayarisha maandiko ya Biblia ya kushiriki naye. Daima uombe wakati wa matembezi. Uamkue kila jamaa na kuwakaribisha kanisani ikiwa hawafiki mara kwa mara. Tumia wakati huu kuzungumza juu ya masomo yaliyopita au swali lo lote ambalo mwanafunzi analo. Ufanye wakati huu kuwa wenye baraka za kiroho kadiri unavyoweza.



c. Waketishe wanafunzi wako katika mviringo. Kufanya hivyo kutawafanya kuona kwamba wao pia ni muhimu kama wengine wo wote darasani. Wataweza kuangaliana uso kwa uso. Hii humtia kila mmoja wao moyo kushiriki katika majadiliano au jambo lo lote la darasa.



d. Hakikisha kwamba unakaa pamoja nao ili waweze kukuona uso kwa uso. Hii ni muhimu sana.

Wakati mwanasiasa anapokwenda mahali fulani, watu humjengea jukwaa (mahali palipoinuka) ili waweze kuwa juu zaidi kuliko watu wengine. Hii ni sawa kwa sababu inaonyesha cheo chake ambacho ni cha juu. Lakini si vizuri kwa mwalimu wa Biblia kuwa juu ya wanafunzi wake. Ainukapo, anaanza kuwa mtawala; hivyo basi inakuwa lazima kwa wanafunzi kumsikiliza, na kutozungumza. Njia nyepesi ya kuanzisha mazungumzo darasani ni kwa mwalimu kuketi chini. Na njia nyepesi tena ya kukatiza mazungumzo ni kwa mwalimu kusimama.


Waalimu wengi hujiona ati hawawezi kufundisha bila kusimama. Labda utahitaji kusimama kuandika ubaoni au kuonyesha picha. Lakini wakati mwingi, mwalimu ataketi chini.

Watu wengi hawataki kufundisha kwa sababu "hawajui majibu yote." Si muhimu kujua majibu yote au baadhi ya majibu. Ni haki kusema, "Swali hilo ni nzuri. Ningependa kujua jibu lake mwenyewe. Nitazungumza na mchungaji (au nitatazama Biblia), kisha nitawaambia jibu juma linalofuata." Lakini, ukianza kuwa mtawala kwa kusimama wakati wa kufundisha na wanafunzi wameketi, ni vigumu kukubali kwamba hujui kila kitu.

Wanafunzi wakiwa wanaketi viti, wewe pia uketi kiti. Ikiwa wanaketi kwenye mikeka au sakafu, wewe pia uketi kwenye mkeka au sakafu. Po pote wanapoketi, wewe pia uketi. Usisimame tu ikiwa ni lazima kufanya hivyo.

e. Tayarisha mapema mahali penu pa mkutano. Wewe kama mwalimu ndiye mwenyeji. Hakuna mtu anayetaka kualikwa kwa nyumba na kuwasili huko bila

kupokewa na mwenyeji wake. Ufike mapema. Tumia dakika chache katika maombi. Panga viti au mikeka. Weka vifaa vyako vya mafunzo tayari. Amkua mwanafunzi wa kwanza kufika kwa kutabasamu (kucheka kidogo) ili aweze kujua kwamba unafurahia kufika kwake.



## UTARATIBU WA NNE: TUMIA MITINDO YA MAFUNDISHO MBALIMBALI NA VIFAA VYA MAFUNZO

Kuna njia nyingi za kufundisha na vifaa vingi vya kutumia katika kufundisha. Haya yote yatazungumzwa katika kurasa zitakazofuata. Mwalimu anayebadilisha mtindo wake na vifaa vyake vya mafunzo mara kwa mara ndiye mzuri. Atawachochea wanafunzi kuja darasani kila Jumapili. Kubadilisha mitindo na vifaa kutafanya mafunzo kuwa ya kuvutia sana.

Katika sura hii tumejifunza maana ya mafunzo na baadhi ya taratibu za mafunzo. Sasa tuko tayari kuona ni watu gani wanaohitaji kufunzwa.

# 3 NI NANI ANAYEHITAJI KUFUNDISHWA?

Kila mshiriki wa kanisa anahitaji kufundishwa, kuanzia mtoto mdogo hadi mzee. Hakuna mtu hata mmoja aliyepita au asiyestahili kufundishwa.

**MTOTO:**

Watoto ndio watu wazima wa kesho. Wakifunzwa leo, watafuata yale waliyojifunza kesho. Tukikosa kuwafunza, basi, kwa kweli, tumeshindwa.

Makanisa mengi yamewaweka watoto wengi katika darasa moja kubwa, kwa mafundisho. Baadhi ya mafunzo haya ni mazuri, lakini zaidi si mazuri sana. Madarasa ni makubwa sana hata mwalimu hawezi kuwafahamu wanafunzi wake kwa majina yao. Hawezi kufuata utaratibu mwema wa mafundisho. Yale anayoweza kufanya ni kutuliza kelele, kuwaongoza watoto kuimba nyimbo chache, kusimulia hadithi na kuwaaga wanafunzi. Mtoto hana nafasi kuzungumza, kuuliza maswali au kushiriki mawazo yake. Baadhi ya wanafunzi huwa wamebeba ndugu zao wadogo. Hawawezi kusikiliza mafunzo kwa sababu wanatunza hao ndugu zao wadogo. Katika hali kama hii; mwanafunzi hujifunza kwa uchache zaidi.

Je, ifanywe nini basi? Pata waalimu wengi. Gawa darasa katika makundi madogo. Weka watoto wenye umri sawa katika darasa moja. Tumia masomo yaliyotayarishwa kwa ajili ya umri wao.

**VIJANA:**

Yatupasa kuwafunza vijana wetu. Utamaduni sasa unaachiliwa mbali; na vijana wanahitaji mambo ya kisasa maishani mwao. Mambo haya yanapaswa kuwa Biblia. Kujishughulisha zaidi katika kuongoza maisha ya vijana leo ni muhimu sana kwa kuwa kanisa huwasaidia katika kujenga maisha mema ya Kikristo kwa ajili ya siku zijazo.

Tangu mwanzo waalimu wawili wanahitajika, mmoja mwanamume kufundisha vijana na mama kuwafundisha wasichana. Majadiliano mengi darasani hufaulu vizuri ikiwa vijana na wasichana wamegawanywa. Kwa kawaida, wasichana huwa huru kabisa wakiwa ndani ya darasa lao wenyewe.

**WAZIMA:**

Wazima wengi makanisani hufikiri ati "Shule ya Jumapili" ni kwa watoto tu. Hufikiri ati hawana haja ya kuendelea kujifunza. Hufikiri ya kwamba msaada wanaopata katika ibada unatosha kumshinda Shetani na kuishi maisha mema ya Kikristo. Hii ni kosa. Wazima wengi makanisani wangali katika hatua ile ya kunywa maziwa (yaani, watoto) (Tazama Waebrania 5:12-14). Bado hawajawa tayari kwa chakula kigumu cha Neno la Mungu.

Majivuno wakati mwingine huwazuia watu wazima kuhudhuria mafunzo ya Biblia. Hawataki kamwe kufikiria kwamba wanahitaji cho chote. Mchungaji anaweza kutenda mengi mno kuondoa wazo hili kwa kueleza hitaji lake mwenyewe la kujifunza. Asifunze darasa ikiwa kuna mtu anayeweza kufundisha. Lakini awe mshiriki wa mojawapo ya madarasa. Watu wazima wakimsikia akieleza mambo anayojifunza, labda watataka kuja kusikia mafunzo hayo.

Ni lazima waalimu wa madarasa kwa wazima wakumbuke kwamba wanawafundisha wazima. Hawawezi kufanywa kama watoto. Ni lazima waalimu wajali wazima katika kila njia inawezekana.

Makanisa mengi yatapata urahisi mwanzoni kuwa na darasa moja tu la watu wazima. Na washiriki wa darasa wanapozidi kuongezeka, darasa linaweza kugawanywa. Labda kina mama watataka darasa lao mbali na wanaume. Au darasa linaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na lugha. Siri ni kuendelea kugawanya darasa kadiri washiriki wanavyoendelea kukua. Hii ndiyo ishara ya kukua na kuongezeka.

## MCHUNGAJI NA VIONGOZI:

Mchungaji pamoja na viongozi wa makanisa wanahitaji mafunzo. Lakini mara kwa mara huwa hakuna nafasi ya mafunzo kwa sababu wao ndio wanafunza wengine. Jibu zuri la shida hii ni kwa mchungaji kuwa na saa katikati ya juma ili kuwafunza waalimu. Anaweza kutumia mafunzo maalum au kufundisha somo la Jumapili inayofuata. Kanisa lo lote lisitosheke na mpango wake wa mafunzo mpaka kila mtu kanisani amepata nafasi ya kushiriki katika mafunzo ya kila juma.

## ASIYE MKRISTO:

Madarasa mengine ya Biblia yana watu wasio Wakristo. Mwalimu atajua hali ya kiroho ya washiriki wake na atafundisha akiwa na kusudi la kumleta kila mmoja kwa Bwana. Walakini, watu wengi wasio Wakristo hawaji kanisani. Tunawafikiaje?

Njia nzuri ya kumfikia mtu asiye Mkristo kwa mafunzo ya Biblia ni kuwa na mafunzo hayo katika


nyumba mbalimbali. Hapo mtu atakuwa na urahisi wa kumjia Bwana. Mawazo mengine ni kuwa na mafunzo ya Biblia hospitalini, gerezani au shuleni.

**NENO LA MWISHO:**

Mipango mingi mizuri zaidi imetayarishwa kwa miaka mingi kutumiwa kuwafunza watu wetu. Baadhi yao ni mafunzo ya Biblia, T.E.E., Bible Way, Uanafunzi na mipango ya kina mama. Hizi zote ni nafasi za kujifunza. Hatuwezi kufundishwa kupita kiasi. Jinsi kanisa linavyotoa mafunzo mengi ndivyo washiriki wetu wanavyokua na kupevuka.









# 4 MAHALI PA KUFUNDISHIA

Mafunzo ya Biblia yanaweza kufanywa mahali pengi.

## KANISA

Mahali pa kwanza ambapo panapasa kufikiriwa ni kanisa. Washiriki wamezoea kuja kanisani kila Jumapili kwa ibada. Ni jambo rahisi kuanzisha darasa la Biblia dakika 30 hadi 45 kabla ya ibada kuanza. Ratiba (utaratibu) inayofaa kufuatwa ndiyo hii:

| | |
|---|---|
| Saa 3:45 asubuhi | Mafunzo ya Biblia kwa wote |
| Saa 4:30 asubuhi | Mwisho wa mafunzo |
| Saa 4:45 asubuhi | Ibada ya Asubuhi |

Mnaweza kutumia ratiba inayowafaa.

## MAHALI PA KUJIFUNZIA BIBLIA

Makanisa mengi yana chumba kimoja tu ambacho ni kikubwa. Machache yana vyumba viwili vidogo. Kwa kawaida hii tu ndiyo nafasi iliyopo. Kanisa halina budi kuwa na nafasi kwa madarasa yote iwapo linataka kufanya kazi nzuri. Wakati wa kujenga kanisa jipya, nafasi ya kutosha kwa mafunzo ya Biblia inapaswa kufikiriwa. Na kwa makanisa ambayo yamekwisha kujengwa, vyumba vya madarasa ya Biblia vinaweza kujengwa. Kabla ya suluhisho la kudumu kupatikana, kanisa linaweza kutumia nafasi nyingine.

Kila kanisa litahitaji kufikiria hali yake lenyewe na kukata shauri, jambo la kufanya. Makanisa mengine yapo katika sehemu zenye watu wengi mno. Watu hao labda watakubali kuwa na mafunzo ya Biblia katika makundi

makundi nyumbani mwao. Washiriki wa madarasa watastahili kukumbuka kuwa wenye adabu na huruma kwa wenye nyumba wanamokutania.

Labda nyumba ya mchungaji inaweza kuwa karibu na kanisa. Labda vyumba kadha katika nyumba yake vinaweza kutumiwa kama madarasa.

Kanisa linaweza kuwa na nafasi chini ya paa yake. Madarasa yanaweza kukaa nje ya kanisa kwenye uvuli au kwenye uvuli wa paa.

Chumba kile kikubwa cha mkutano kinaweza kugawanywa ili madarasa kadha yakutane humo. Yagawanywe kwa nafasi zaidi ili madarasa yakutane humo bila msongamano wo wote.

Mawazo mengine yatawajia wale wanaotafuta uongozi wa Mungu kupata nafasi za madarasa ya Biblia.

**NYAKATI MBALIMBALI ZA KUKUTANA:**

Kadiri madarasa yanayoendelea kukua na kugawanywa, ndivyo nafasi huongezeka kuwa ndogo. Labda mpango huu mwingine unaweza kuwa mzuri, yaani, ule wa kufundisha madarasa nyakati zingine. Masomo yanaweza kufanywa Jumapili adhuhuri au jioni au siku nyingine yo yote ya juma. Baadhi ya madarasa kukutana wakati mmoja, na mengine wakati tofauti. Kwa kweli, suluhisho hili si zuri kwa shida ya nafasi, lakini labda inaweza kuwa la maana ikiwa hakuna njia nyingine.

**KIJIJINI AU MJINI:**

Mbali na kanisa kuna mahali pengi pa kukutania kwa madarasa ya mafunzo ya Biblia. Washiriki wanaweza kutafuta nafasi hizi baada ya mpango mzuri wa mafunzo

katika kanisa kuwa unaendelea. Waalimu wanaofunza Jumapili na wengine wanaweza kutafuta mahali pazuri pa kukutania katika majengo ya kawaida.

**HOSPITALINI:**

Hospitali nyingi hufurahia kuwakaribisha makundi ya kanisa kuja kujifunza masomo ya Biblia. Wagonjwa wengine ni wale wa kukaa siku nyingi hospitalini na hufurahia mafunzo ya Biblia. Ili kuanzisha mpango kama huo, mwalimu au mchungaji aende kwa msimamizi wa hospitali kuzungumza naye. Inawapasa kujua hasa yale wanayotaka kufanya na jinsi watayafanya. Ni lazima wasikilize madokezo ya mkuu yule wa hospitali. Kisha watapatana juu ya wakati na chumba cha kukutania. Hatimaye kanisa lihakikishe kwamba mwalimu anawahi mahali pale kila wiki.

**GEREZANI:**

Mafunzo ya Biblia yanaweza kufanywa gerezani. Idhini iombwe kutoka kwa wakuu wa gereza. Anzisha mafunzo ya Biblia gerezani ikiwa kanisa lina uhakika wa kuendeleza mafunzo hayo. Ikiwa unataka kufundisha kwa muda fulani tu, kama miezi sita tu, basi mnaweza kupanga.

**NYUMBANI:**

Mafunzo ya Biblia nyumbani ni muhimu kwa wale ambao hawawezi kuhudhuria kanisa kwa sababu ya ugonjwa, kazi au shida nyingine. Kanisa linaweza kuwafikia watu wa madhehebu mengine nyumbani mwao. Uliza ili mwanzishe mafunzo ya Biblia nyumbani mwa washiriki. Tafuta mwalimu. Waalike majirani. Mengi ya mafunzo hayo ya Biblia nyumbani huzaa makanisa.

# MAHALI PO POTE:

Madarasa ya mafunzo ya Biblia yanaweza kufanywa mahali po pote. Hitaji la pekee ambalo lahitajika ni waalimu wanaojitolea.

## 5 KWA NJIA GANI?

Kwa wengi, shida kubwa ya kuanzisha mpango mzuri wa mafunzo ya Biblia ni kutojua jinsi ya kufanya. Darasa huanzishwaje? Somo hutayarishwaje? Vifaa vya mafunzo hutoka wapi na huagizwa kwa njia gani? Vifaa gani vya mafunzo vinavyotumiwa? Vifaa hivyo hutengenezwaje? Ni njia zipi za mafunzo ya Biblia zinazofaa?

Majibu ya baadhi ya maswali hayo yanatolewa katika sura hii. Vifaa vya mafunzo vitajadiliwa katika sura ya sita na njia au mitindo katika sura ya saba.

### KUANZISHA DARASA LA BIBLIA:

Kuanzia wakati Yesu alipoweka kando vifaa vyake vya useremala na kuanza utumishi wake hapa duniani, Yesu alikuwa mwalimu. Alifundisha sinagogini, hekaluni, nyumbani mwa marafiki, njiani na milimani. Yesu alikuwa mwalimu na alituachia mfano wake kufuata. Alipomaliza wajibu wake, aliwaamuru wanafunzi wake kuendelea kufundisha mafunzo yale aliyokwisha kuanzisha. Huu ni wajibu mkubwa, lakini ni furaha!

Hatua ya kwanza kuanzisha darasa la Biblia ni kupokea wajibu huu ambao Yesu alitupa. Tunapokea kazi ya kufundisha, Mungu anapotutayarishia njia. Kujitoa hasa ni kati ya mwalimu na Mungu.

Kwa kuwa mipango yote ya kanisa ni wajibu wa kanisa zima, ni juu ya kanisa kuamua wale watakaofunza katika mipango yake ya mafunzo ya Biblia. Walakini, ukijisikia kwamba Mungu anakuongoza kufundisha, unahitaji kumwambia mchungaji. Ataleta jina lako mbele ya kamati ya kanisa au kanisa zima. Atakusaidia kufanya mipango yako.

Baada ya shauri kukatwa, mwalimu aamue kwamba atafundisha kina nani. Hii ni hatua ya pili. Ikiwa darasa hili ndilo la kwanza ambalo kanisa linalo, mchungaji anaweza kukata shauri liwe la watu wazima. Kwa kweli, haijalishi ni darasa gani linaloanzishwa kwanza.

Hatua ya tatu ni kumtafuta mwanafunzi wa kwanza. Ikiwa darasa hili la Biblia ndilo la kwanza la kanisa fulani, kazi ya mwalimu itakuwa rahisi. Atakuwa akiwafundisha wanafunzi wale ambao wamekuwa wakihudhuria. Matangazo mafupi wakati wa ibada ya asubuhi itawafahamisha wanafunzi wanaotaka kujiunga na mafunzo kujua wakati na mahali ambapo darasa jipya litakutana. Makanisa mengi yataanzishwa kwa njia hiyo. Labda mwalimu anaweza kukata karatasi kubwa yenye maandiko na kuibandika kwenye mlango wa kanisa pia.

Walakini, ikiwa darasa ni la wale ambao kwa wakati huu hawahudhurii kanisa, mwalimu hana budi kwenda kuwatafuta wanafunzi wake wa kwanza. Anaweza kutangaza kanisani ili washirki wakawaambie wengine. Kisha atahitaji kubandika makaratasi yale makubwa yenye maandiko kwenye mahali ambapo wanafunzi wanaotaka kujiunga wanaweza kuyaona. Karatasi kubwa yenye maandiko ikibandikwa sokoni inaweza kuwavutia wanawake, na nyingine shuleni inaweza kuwavutia vijana au watoto. Pamoja na hayo, mwalimu awatembelee wanafunzi wale wanaotaka kujiunga na awakaribishe kuja darasani.

Baada ya shauri kukatwa, kwamba darasa litakuwa la kundi fulani, na wanafunzi wa kwanza kupatikana, mwalimu achukue hatua ya nne na atayarishe somo lake la kwanza. Kuna hatua nne muhimu za kufuata.

a. Chagua kusudi la mafunzo.

Masomo yaliyotayarishwa vyema yatakuwa na kusudi. Mwalimu anaweza kutumia kusudi hilo au lingine analochagua. Ikiwa amekwisha kupeleleza vyema hitaji maalúm katika darasa lake, anaweza kujaribu kutimiza hitaji hilo katika somo lake. Hilo ndilo kusudi lake. Mfano mmoja wa kusudi ni, "Kuwaongoza wanafunzi katika ufahamu wa Yesu." Mfano mwingine unaweza kuwa, "Kulitia darasa langu moyo kutumia wakati mwingi katika maombi." Kusudi linapasa kuelezwa waziwazi na kwa kifupi. Mafunzo yote ni lazima yatimize kusudi hilo.

Ni vigumu sana kupima mafundisho yetu. Je, tumefikia kusudi la mafunzo yetu? Kwa mfano, je, mwanafunzi anafahamu kamili zaidi kwamba Yesu yu nani? Je, hutumia wakati mwingi katika maombi? Kusudi ndilo lengo kubwa ambalo mafunzo yote yanalenga.

b. Chagua shabaha ya somo.

Kama kusudi, shabaha, ni malengo ambalo mwalimu hujaribu kufikia kwa somo lake. Walakini, shabaha ni tofauti na kusudi kwa sababu yanaweza kupimwa. Tofauti nyingine ni kwamba mwalimu atakuwa na kusudi moja tu lakini, atakuwa na shabaha chache. Kwa mfano, ikiwa kusudi la somo ni kumjua Yèsu, shabaha inaweza kuwa:

1) Kwamba wanafunzi wataweza kukariri Mathayo 16:16.

2) Kwamba wanafunzi watasema katika maneno yao wenyewe kwamba kazi ya Yesu hapa ulimwenguni ilikuwa nini.

3) Kwamba wanafunzi watachora picha kuhusu jinsi wanavyofikiria sura ya Yesu ilibadilika na kung'aa mlimani.

Shabaha hii itaweza kupimwa na mwalimu. Wakati wa kufundisha, mwalimu atatoa nafasi kwa wanafunzi kuonyesha ujuzi wao kwa kufanya baadhi ya mambo ambayo yamo katika shabaha.

c. Chagua mtindo au njia ya mafundisho.


Kwa kukumbuka kusudi na shabaha, mwalimu atachagua mtindo au njia ya kufikia kusudi la somo. Vifaa vilivyotayarishwa vyema vitatoa njia, lakini itakuwa juu ya mwalimu kuchagua njia au mtindo anaotaka.


d. Chagua vifaa vya mafunzo.

Kumbuka ya kwamba milango zaidi ya mawasiliano ambayo mwanafunzi hutumia kulielewa somo ndiyo humsaidia kujifunza vizuri zaidi. Vifaa vya mafunzo hufanya kujifunza kuwa kwa maana zaidi.

Hatua nne katika kuanzisha darasa la Biblia ni:

1. Kubali wajibu.
2. Kata shauri juu ya kundi ambalo darasa litakuwa nalo.
3. Watafute wanafunzi wa kwanza.
4. Tayarisha somo la kwanza.





## VIFAA

Mwalimu akiwa na Biblia, anavyo vifaa atakavyofundishia. Kuandika somo kutoka Biblia ni ngumu zaidi kuliko kutumia somo ambalo umekwisha kutayarishiwa. Walakini mpaka vifaa vinaweza kuagizwa na kupokelewa, Biblia itamsaidia mwalimu katika mafunzo yake.

Waalimu wapya watafanikiwa sana wakitembelea "Baptist Publications" kuchagua vifaa vya kutumia. Huko watapata masomo yaliyokwisha kuandikwa, hasa kwa wanafunzi wa darasa lao. Unaweza kununua vifaa vya mafunzo kama picha. Wauzaji vitabu huko watawaelezea jinsi vitabu vinaweza kuagizwa na kutumiwa. Pia watawaonyesha jinsi vitabu vinavyopangwa ili sehemu fulani za Biblia ziweze kusomwa kwa wakati fulani.

Ikiwa waalimu hawawezi kutembelea "Baptist Publications," wapate anwani zao kutoka mchungaji wao. Wawaandikie ili wawatumie kitabu chenye orodha ya vitabu vyao. Wawaulize ili wawaeleze tofauti za mafunzo kulingana na umri. Watume agizo lao haraka ili waanze kutumia vitabu hivi vilivyotayarishwa.

# 6 MISAADA YA MAFUNZO

Yesu ndiye aliyekuwa Mwalimu mkuu. Wanafunzi wake walifahamu mafunzo yake kwa urahisi. Mafunzo yake yalijaa mambo kama nira, mbegu, kondoo, mbwa mwitu na vitu vingine ambavyo watu walivitumia katika maisha. Siku moja aliwaambia wasikilizaji wake kuinua macho yao kuona jinsi mavuno yalikuwa tayari. Alijua kutumia vitu ambavyo watu walifahamu ilifanya mafundisho yake kuwa dhahiri au wazi. Tuna mfano mzuri sana wa kufuata.

Unaweza kununua misaada ya mafunzo katika miji mikuu. Lakini katika miji midogo na vijiji ambako waalimu wengi wa Biblia wako, misaada ya mafunzo siyo rahisi kupata. Kwa kawaida, karatasi, kalamu za mate, za rangi na gundi hupatikana. Unaweza kutengeneza vifaa vingi na vitu hivi.

## PICHA


Picha ni msaada mzuri sana wa kufundishia. Pata picha nzuri kutoka magazetini kwa kuzikata na kuzibandika kwenye karatasi kubwa nyeupe. Chagua picha kubwa badala ya ndogo, kwa sababu darasa lako litaweza kuziona vyema zaidi. Upange kuziweka sandukuni vizuri. Au unaweza kufingirisha.

Si lazima kwa waalimu kujua namna ya kuchora picha. Anaweza kuchora mistari na miviringo kumaanisha picha za watu na wanyama. Jaribu hii:


Chora mviringo kuwa kichwa.
Ongeza mstari kuwa mwili.
Chora mistari minne kuwa mikono.
Chora mistari sita zaidi kuwa miguu.
Fanya mazoezi ya kumchora mtu huyu.
Sasa umvalishe.




Chora mistari mingine kuwa shati
Chora mistari mingine kuwa suruali.
Umvalishe viatu.
Ongeza mistari mingine kwa mikono na shingo.
Futa mistari ya ndani.



Chora mwanamke.




Chora picha ya mtu ye yote anayetajwa katika Biblia.




## Jaribu kuchora picha za watu katika mtindo tofauti.

Endelea kufanya mazoezi.



Chora picha kamili ya mtu anayetajwa katika Biblia.



Endelea kufanya mazoezi ya michoro kama hii.


Ni vizuri kuchora picha mapema ili iwe tayari kwa somo. Tumia karatasi au ubao wa kuandikia. Masomo mengine yanaweza kufundishwa wakati wa kuchora picha. Fanya mazoezi ya kuchora kabla ya darasa kuanza.

Tumia picha kuchangamsha mazungumzo, kueleza ukweli, kutoa habari au kuanzisha somo jipya. Mwanafunzi akisikia na kuona, hataweza kusahau.

## RAMANI AU MAKARATASI MAKUBWA YENYE MAANDIKO

Ramani au makaratasi makubwa yenye michoro ni ya muhimu sana kwa mwalimu. Uzitumie kutoa habari muhimu katika maneno machache tu. Uzitayarishe mapema na kuzitumia unapozihitaji masomoni. Ongeza picha katika ramani yako. Tayarisha mfululizo wa ramani na kuziweka pamoja na kamba nyembamba. Ufungue-fungue kurasa za ramani wakati unapofundisha.

1. Tumia ramani kutangaza tukio linalofuata. Ramani ifuatayo ni mfano wa mpango wa mkutano wa vijana.



2. Tumia ramani kufundisha hatua ya mfululizo wa matukio katika somo. Ramani hizi zinaweza kukusaidia kuhusu hatua za wokovu, jinsi ya kushuhudia, safari za Paulo za umisheni, au juma la mwisho la Yesu hapa duniani.

3. Tumia ramani kufundishia utaratibu wa vifaa kama vitabu vya Biblia, majina ya Mitume au majina ya wanawake wa Biblia.

4. Tumia ramani kufundishia vifungu vya Biblia, hasa kifungu cha kukumbuka.

5. Tumia ramani kuorodhesha mambo muhimu.

6. Tumia ramani kuonyesha vile saa zinafuatana.

Usiweke maelezo mengi katika ramani yako. Andika maandishi makubwa ili uweze kuyasoma hata ukiwa mbali. Uandike katika mistari iliyonyoka. Tumia kalamu za rangi mbalimbali ili ramani yako iwe na rangi aina tatu hivi. Tumia ramani kisha uiondoe. Usiiache kwa muda mrefu.

**RAMANI ZA NCHI**

Ramani ni chombo cha muhimu sana kwa mwalimu wa Biblia. Unaweza kuzinunua katika duka la vitabu. Au zinaweza kutengenezwa kwa urahisi kwa karatasi kubwa na kalamu ya mate. Biblia zingine zina ramani nzuri. Panua ramani hizi ili darasa lote liweze kuziona. Unaweza kufuata mtindo huu kupanua ramani ndogo Bibliani kuwa kubwa.


1. Gawanya ramani ndogo katika vipande vyenye ukubwa sawasawa vidogo.

2. Gawanya karatasi kubwa katika vipande vyenye idadi sawa na ramani ndogo. Vipande hivi vitaonekana vikubwa.


3. Kuanzia upande wa kushoto juu, uchore mambo yale yanayotakiwa.

4. Ufanye vile vipande vyote sawa.

ramani ndogo



ramani kubwa



5. Futa alama hizo za mistari.


6. Tumia kalamu za rangi kuipaka ramani.

7. Baada ya kuitumia, uweke ramani hiyo katika mahali pa usalama ili itaweza kutumiwa tena baadaye.

**VITU VYA KAWAIDA**

Waalimu watapata vitu vingi vya kutumia ambavyo ni vya kawaida. Vitu hivi vinaweza kuleta maana sana kwa somo. Kuhusu somo juu ya muumbo, mwalimu anaweza kutumia maua, mawe, maji na majani. Kuhusu somo juu ya Daudi aliyemwua Goliathi unaweza kutumia kombeo.


Tengeneza picha za vitu kwa kutumia karatasi. Chora picha ya mti kisha uikate uibandike picha kwenye karatasi nzito na uisimamishe.




Utumie mifano na vitu hasa unapowafundisha watoto darasani. Watoto hupenda sana kuona vitu hivi.

## VIFAA VINGINE VYA MAFUNZO

Tayarisha karatasi ndefu kwa kuunganisha pamoja vipande vipande vya karatasi. Kisha uvigawe vipande hivyo na kuchora picha. Picha hizo zapasa kusimulia hadithi unayofundisha.




Tumia grafu kuonyesha mahudhurio na majina ya wanafunzi wanaokariri maandiko au kweli zingine.

Ikiwa una ukanda wa kunasia sauti; uitumie darasani. Huvutia sana wanafunzi. Usifundishe somo lote kwa ukanda ule, bali sehemu tu.

"Flannelgraphs" ni vifaa vizuri kutumia. Walakini, unahitaji ustadi kutumia. Unaweza kununua hadithi mbalimbali zimetayarishwa. Kutengeneza "flannelgraphs" uchore picha kwa karatasi, zipake rangi, zikate kwa mistari na zibandike kwa gamu kwa kitambaa maalum, jina lake "flannel."

Tumia mawazo yo yote unayoweza kufikiria. Uyatumie uone kama yanafanya kazi. Tumia kila wazo kama unavyoweza.

# 7 NJIA ZA KUFUNDISHA

Yesu alipenda kusimulia hadithi. Alifurahia kujadiliana pamoja na wanafunzi wake. Alipenda mahojiano. Alikuwa shupavu kutumia maswali na majibu kufundisha ukweli. Kusimulia hadithi, majadiliano, mahojiano, maswali na majibu, kila moja ni njia ya kufundisha. Yesu aliyatumia yote kuwasilisha ujumbe kwa wasikilizaji wake. Sisi pia twaweza kutumia njia mbalimbali kuyafanya mafundisho yote kuwa ya kuvutia.

Mafundisho ya Biblia, mara kwa mara yanaweza kufundishwa katika njia nyingi mbalimbali. Kufahamu njia ya kutumia na kuitumia vyema kutaendeleza sana mafundisho yako. Unapojifunza njia hizi, ufikirie kweli za kiroho au hadithi za Biblia ambazo zinaweza kufundishwa kwa mojawapo ya njia hizi.

## KUSIMULIA HADITHI

Kusimulia hadithi ni njia moja ambayo imepata kutumiwa sana barani Afrika kuanzia kuzazi kimoja hadi kingine. Ingawa kusimulia hadithi hufurahisha, ni sehemu muhimu sana ambayo imeweza kuhifadhi mila.

Kila mtu hufurahia kusikiliza hadithi nzuri inayosimuliwa na msimulizi wa hadithi hodari. Watu wazima na vijana wanapenda hadithi sawa na vile watoto wanavyopenda. Sehemu ya mahubiri ambayo mara kwa mara mtu huweza kukumbuka ni hadithi ambayo mhubiri alitumia kufundishia ukweli.

Simulia hadithi iwapo somo unalofundisha lina hadithi. Sehemu kubwa ya Biblia ni hadithi. Tumia hadithi za maisha ya kila siku, kufundisha ukweli wa somo lako.

## UZURI WA KUSIMULIA HADITHI

1. Njia hufurahisha wanafunzi.

2. Wanafunzi wako watakumbuka maelezo mengi na matukio.

3. Utawachochea wanafunzi kimawazo.

4. Mwanafunzi anaweza "kuona" hadithi unayosimulia akilini mwake.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

Kwa sababu msimulizi hodari wa hadithi huifanya njia hii kuonekana rahisi, waalimu wengine hushindwa kujitayarisha vya kutosha. Kusimulia hadithi kwa njia nzuri huhitaji mazoezi na matayarisho ya kutosha. Baadhi ya makosa ya kawaida ni:

1. Kuacha nje sehemu za hadithi zinazovutia.

2. Kuongeza maelezo mengi kupita kiasi.

3. Kutumia lugha au maneno ambayo wanafunzi hawaijui.

4. Kusoma hadithi badala ya kuisimulia.

5. Kuigeuza hadithi.

## UTARATIBU WA HADITHI NZURI

1. Jitayarishe vyema daima. Fanya mazoezi ya hadithi mara kadha nyumbani. Hakikisha kwamba unakumbuka sehemu zote za hadithi na mambo yake muhimu. Usitegemee maandiko ya hadithi.

2. Kuwa mwenye furaha katika matayarisho yako. Simulia hadithi kana kwamba unaifurahia kama wasikilizaji wako.

3. Tumia vidole, mikono na sura yako kusimulia hadithi. Jihusishe katika kusimulia.

4. Tumia macho yako kama mawasiliano. Mfanye kila mwanafunzi kujisikia kana kwamba ni yeye tu anayesimuliwa hadithi hiyo.

5. Inua sauti yako juu kidogo ili kila mwanafunzi aweze kuisikia. Uinue na kushusha sauti yako wakati unaposisitiza jambo. Tumia matamshi mbalimbali katika njia sawa na hiyo. Kusimama maneno yako kwa muda bila kupumua ni vizuri.

## HOTUBA

Labda njia ya kawaida ya kufundisha ni ya hotuba. Hata waalimu wengine hufikiri ati hiyo ndiyo ya pekee. Hotuba nzuri ni mafundisho mema, lakini kuitumia sana au kuitumia vibaya tena ni mafundisho mabaya.

Unaweza kutumia hotuba katika kufundisha Biblia katika njia mbalimbali. Hutubia juu ya maombi. Fundisha historia fupi ya wateule wa Mungu. Tumia hotuba kueleza safari za Paulo za umisheni. Hutubia juu ya Kristo katika Agano la Kale au Waamuzi na kazi zao.

Hotuba ni njia ambazo mwalimu tu ndiye anayezungumza. Hotuba ina uzuri wake na ubaya wake. Mwalimu mwema atatumia njia hii mara kwa mara.

### UZURI WA HOTUBA

1. Unaweza kutoa habari nyingi katika muda mfupi.

2. Unaweza kuwahutubia makundi madogo na makubwa.

3. Hauhitaji matayarisho mengi kama njia nyingine.

4. Unaweza kulinganisha ukweli wa Biblia na maisha ya kila siku kwa uràhisi.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Hotuba inaweza kumchosha mwanafunzi haraka.
2. Hakuna njia yo yote ambayo kwayo mwalimu anaweza kupima iwapo wanajifunza kweli.
3. Mwanafunzi anaweza kumfikiria mwalimu kama mwenye mamlaka ya mwisho.

## UTARATIBU WA HOTUBA

1. Fuata utaratibu uliopangwa vizuri.
2. Tegemeza hotuba yako kwa vifaa vizuri vya kufundisha.
3. Tumia mifano mizuri ya maelezo.
4. Unganisha utaratibu huu na mwingine.
5. Tumia macho yako kama mawasiliano, tena utumie sauti nzuri na misemo mizuri.

## MAJADILIANO


Majadiliano ndiyo mojawapo ya njia nzuri zaidi ya kuwafundisha watu wazima na vijana. Inatoa nafasi kwa kila mwanafunzi kushiriki. Mwalimu mwerevu anaweza kutumia njia hii kuwawezesha wanafunzi kutoa maoni yao hata yule asiyependa kuzungumza darasani.

Wakati wa majadiliano, mwalimu akiwa katika mviringo pamoja na wanafunzi wake; aulize swali

(litakalomfanya kila mwanafunzi kufikiri na kujibu katika maneno mengi badala ya kusema ndiyo au hapana). Angojee majibu. Labda anaweza kuita majina ya wanafunzi ili kuwahusisha zaidi katika majadiliano. Kwa mfano aseme, "Sulemani, unaweza kueleza maana ya Mkristo kuwa chumvi ya ulimwengu?" Mwalimu asiye msemaji zaidi kuliko wanafunzi. Asikilize kwa makini. Baadaye anaweza kutaka kusahihisha jambo lililosemwa ikiwa darasa halikufanya hivyo. Aongoze darasa kufikia lengo au kusudi la somo.

Kundi la majadiliano huonekana kama picha zifuatazo. Kundi la kwanza, kisha lingine lijadiliane. Mwalimu asiwe msemaji sana wa majadiliano.







Majadiliano hayawi ya mtu mmoja bali ni ya kundi zima. Mazungumzo yanayofuata:

Majadiliano Yanayofuata:

Mwalimu Nyaga: Tumekuwa tukijifunza maisha mapya katika Kristo kwa muda wa wiki kadha. Somo letu la leo tutajifunza juu ya Neno la Mungu. Jinsi gani tuliipata Biblia?

Bwana Kamau: Una maana ya kwamba Bibilia hizo tulizo nazo sasa?

Bwana Karisa: Ndiyo, lakini nafikiri ana maana ya kwamba jinsi tulivyopata Biblia kutoka kwa Mungu.

Mwalimu: Hiyo ni kweli. Mungu alitupaje Neno lake?

Bwana Njoroge: Mungu alimpa Musa Neno lake katika mlima Sinai. Musa alikwenda huko, akakaa mpaka Mungu alipompa Biblia.

Bwana Kamau: Lakini haikuwa Biblia yote, sivyo?

Bwana Njoroge: Nafikiri ilikuwa yote.

Bwana Simon: Sikubaliani nawe, Ndugu. Vitabu vingi vya Biblia viliandikwa baada ya Musa kushuka mlimani. Biblia inatueleza juu ya kuzaliwa kwa Yesu. Hayo yalifanyika baadaye sana.

Bwana Njoroge: Ndiyo, lakini Mungu alijua kwamba mambo hayo yangefanyika. Anajua kila kitu.

Bwana Samweli: Hiyo ni kweli. Mungu ajua kila kitu lakini sidhani kwamba Mungu alimpa Musa Biblia nzima. Baadhi ya vitabu vya Agano Jipya viliandikwa na Paulo.

Bwana Kamau: Kimoja kiliandikwa na Mathayo na kingine kiliandikwa na Petro, sawa Bwana Nyaga?

Mwalimu: Ndiyo, Bwana Kamau. Umesema ukweli.

Bwana Njoroge: Ikiwa waliandika baadhi ya vitabu vya Biblia, basi, Musa alileta vitabu gani?

Bwana Simon: Alileta Amri Kumi za Mungu. Lakini waandishi wengine kama Paulo walijuaje mambo ya kuandika?

Bwana Karisa: Mungu aliwaambia mambo ya kuandika.

Bwana Njoroge: Je, wote walipanda mlimani kama Musa?

Bwana Mwenjes: La, hasha. Waliandikia katika mahali walimokuwa. Mungu aliwaambia mambo ya kuandika katika kila mahali walimokuwa.

Bwana Njoroge: Kwa jinsi gani? Je, walisikia sauti iliyoelezea kila neno walilostahili kuandika?

Mwalimu: Hilo ni swali zuri.

Bwana Karisa: Mungu aliwaongoza kwa Roho Mtakatifu.

Bwana Njoroge: Yaani, maana yako ni nini?

Bwana Karisa: Je, unajua jinsi Roho Mtakatifu anavyokwambia kufanya jambo? Alisema na waandishi katika njia sawa na hiyo.

Mwalimu: Hilo jibu zuri. Mungu hutuongoza leo kwa njia ya Roho Mtakatifu. Alitumia njia hiyo hiyo kuwaongoza waandishi wa Neno lake.

Ingawa majadiliano haya hayajaisha, yanaonyesha jinsi mwalimu anavyopaswa kuongoza majadiliano. Tumia majadiliano kuanzisha au kufunga somo. Masomo mengine yanaweza kufundishwa katika njia sawa na hiyo.

## UZURI WA NJIA YA MAJADILIANO

1. Kila mmoja anaweza kushiriki mawazo yake.
2. Kundi linaweza kusahihisha makosa badala ya mwalimu.
3. Wanafunzi watapendezwa tena watafurahia somo.

4. Wanafunzi wataanza kuwa na roho ya umoja katika kundi watakapotambua kwamba kila mmoja anashiriki mawazo yake.

5. Mwalimu atajua mara moja kama wanafunzi wameshika ukweli wa mafundisho yake.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Mwalimu asipokuwa macho, darasa linaweza kuacha somo na kuanza kujadiliana mambo mengine.

2. Unaweza kumwaibisha mwanafunzi ukimlazimisha kushiriki. Mwalimu awafahamu wanafunzi wake na asiwalazimishe kusema cho chote kama hawana la kusema.

3. Usitumie njia hii kwa kundi kubwa. Ni wachache tu watakaoshiriki. Majadiliano ya aina nyingine iitwayo kundi la vuma yanaweza kutumiwa kwa kundi kubwa.

## TARATIBU KATIKA MAJADILIANO MAZURI

1. Hakikisha kwamba swali lako ni dhahiri na litawafanya wanafunzi kufikiri.

2. Swali ni lazima liambatane na kusudi la somo.

3. Jitayarishe kuwa mshiriki katika majadiliano badala ya kuwa msemaji.

4. Waonye wanafunzi wanaosema zaidi kuliko wengine. Kusema "Asante sana, Esta, kwa mawazo yako. Nafikiri Fatuma sasa angependa kushiriki mawazo yake," kutasaidia sana hapa.


5. Kwanza wanafunzi hawataweza kujua jinsi ya kujadiliana katika darasa la Biblia. Kwa kawaida,

wamekuwa wakisikia hotuba tu, kwa hiyo watajua kusikiliza tu. Mwalimu anaweza kutumia muda fulani kuwaonyesha jinsi kushiriki katika majadiliano.

## MAKUNDI YA VUMA

Makundi ya vuma ni aina nyingine ya majadiliano. Mwalimu aligawe kundi lake katika vikundi vidogo kisha akipatie kila kikundi jambo la kuzungumziwa. Vikundi hivi vitakutana kwa wakati uliopangwa, kisha walete ripoti katika kundi kubwa.

Labda picha ya makundi ya vuma inaweza kuonekana hivi:



## UZURI WA MAKUNDI YA VUMA

1. Vikundi vidogo huwa na nafasi kubwa ya majadiliano.
2. Mambo mengi yaweza kuzungumzwa kwa muda mfupi.
3. Wanafunzi wanaoona haya wanakuwa na moyo wa kushiriki zaidi katika kikundi kidogo kuliko kikundi kubwa.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Labda wanafunzi wengine wanaweza kutumia nafasi zaidi kuliko wengine.
2. Kila kundi liwe na wanafunzi saba au wachache.
3. Usiruhusu vikundi vingine kutumia wakati zaidi huku wenzao wakiwangojea mpaka wamalize.
4. Mara kwa mara kundi litakoma majadiliano na hukumu isiyo kweli.

## UTARATIBU KATIKA MAJADILIANO YA MAKUNDI YA VUMA

1. Tayarisha mambo ya kuzungumziwa kabla ya wakati kufika. Hakikisha kuwa yamepangwa vizuri.
2. Kuwa na muda wa kupanga viti au mikeka.
3. Hakikisha kwamba kila kundi lina kiongozi na mwandishi. Kiongozi ataongoza majadiliano na mwandishi ataandika na kutoa ripoti kwa kundi zima.
4. Weka muda maalum wa kuanzia na kumalizia mikutano.

5. Tembelea kila kundi kuona kwamba kila mmoja anapewa nafasi ya kushiriki, kuona kama masomo yale ni dhahiri na kuwatia moyo.

6. Kuwa na muda wa kutosha kusikiliza ripoti kutoka kwa kila kundi.

7. Panga somo la muda wa dakika 45 kama ifuatavyo:


   Dakika 10 ziwe za kugawa kundi na kupanga viti.
   Dakika 15 ziwe za vikundi vidogo kukutana.
   Dakika 20 ziwe za kusikiza ripoti kutoka kwa makundi.

8. Wakati ripoti zinapotolewa, uongeze maneno yako au masahihisho.

## MASWALI NA MAJIBU

Njia hii ya mafundisho mara kwa mara huchanganywa na njia ya hotuba kama mtindo wa marudio mwishoni mwa somo. Hiyo siyo njia ya pekee ambayo mtindo na majibu mwalimu anaweza kutumiwa. Mwalimu anaweza kutumia utaratibu mzuri wa maswali kufundisha somo zima.

Mtindo mzuri wa kufuata ni kwamba mwalimu aulize swali na mwanafunzi ajibu. Akitosheka na jibu hilo, aulize swali la pili. Ikiwa ni sivyo, amwulize mwanafunzi mwingine swali la kwanza au aongeze mambo fulani katika swali hilo na kumwuliza mwanafunzi yule wa kwanza.



## UZURI WA MASWALI NA MAJIBU

1. Tumia njia hii muda wa kufundisha ukiwa mfupi.
2. Maswali na majibu huwavuta wanafunzi kushiriki.
3. Wanafunzi watatumia ujuzi wao kujibu maswali na tena wataongeza ufahamu wao.
4. Mwalimu aongoze maswali, majibu kuelekea kusudi la somo.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Kutumia njia hii kila wakati kitachosha wanafunzi.

2. Tumia maswali ambayo kuna majibu zaidi kuliko "ndiyo" au "la".

## TARATIBU KATIKA MASWALI NA MAJIBU MEMA

1. Tayarisha maswali yako mapema ukifuata mfano wako wa matayarisho.

2. Uliza maswali darasani au utoe makaratasi yenye maswali hayo kwa wanafunzi wako mapema iwezekanavyo ili wawe tayari kujibu.

3. Maliza somo lako kwa marudio mafupi ya "Mambo tuliyojifunza leo."

## MAJADILIANO YA KUNDI

Hii ni njia ya nne ya majadiliano. Kundi dogo la watu lialikwe kukaa mbele ya darasa na kuendelea na majadiliano. Majadiliano haya yawe ya kundi tu. Labda mle katika kundi mnaweza kuwako wageni walioalikwa au watu wa darasani. Jambo la kujadiliwa litolewe mapema ili wajitayarishe kujadiliana. Labda sehemu mbalimbali za jambo hilo la kujadiliwa lipewe kila mwanafunzi wa kundi lile la majadiliano. Mwalimu au kiongozi ye yote aliyechaguliwa aongoze majadiliano hayo.

## UZURI WA MAJADILIANO YA KUNDI

1. Habari zaidi zinaweza kutolewa kwa muda mfupi.

2. Darasa hufaidika kutokana na matayarisho ya majadiliano ya kundi.

3. Wanafunzi huvutiwa sana na matayarisho kama haya.



**MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)**

1. Baadhi ya washiriki wa majadiliano ya kundi wanaweza kukosa kuwa na mambo muhimu ya kusema au wanaweza kuchosha kwa matoleo yao.

2. Wakati wa majadiliano labda kundi hawatakubaliana juu ya mambo yale ya kumalizia.

## TARATIBU ZA MAJADILIANO MEMA YA KUNDI

1. Uwafikirie washiriki wa kundi la majadiliano. Je, wana ujuzi wa kazi? Je, watashiriki kikamilifu?
2. Uwaalike mapema ili wawe na wakati kujitayarisha.
3. Uliambie darasa mapema juu ya jambo litakalozungumzwa.
4. Ongoza kundi kufikia mwisho wenye suluhisho.
5. Uwe na wakati mwishowe wa kuyarudia mambo yale mengine yaliyopatikana.
6. Uwaruhusu wasikilizaji kuuliza maswali.

### HADITHI ILIYOTUNGWA KUIGIZWA

Tutajadiliana juu ya hadithi iliyotungwa kuigizwa chini ya vichwa vifuatavyo: Mchezo wa kuigiza, mchezo, mtungo na kiigo cha kuchekesha.

### MCHEZO WA KUIGIZA

Kusudi la mwalimu katika mchezo wa kuigiza ni kuwafanya wanafunzi "kujisikia" jinsi mwingine anavyojisikia. Mwalimu awaambie wanafunzi mbalimbali kushiriki katika mchezo huu akiwa na lengo la kuona jinsi wanavyojisikia. Mfano mzuri wa jinsi ya kutumia njia hii ni kuigiza hadithi ya mwana mpotevu. Baadaye, kila mwanafunzi aliyeshiriki aulizwe, "Je, ulijisikiaje juu ya baba yako ulipoona kwamba amekusamehe?" au "Je, wewe kama baba, ulijisikiaje? Je, ilikuwa vigumu kukubali mambo ambayo mwanao alifanya?" Mfano mwingine utakuwa ni kuigiza hadithi ile ya Msamaria mwema.

## UZURI WA MCHEZO WA KUIGIZA

1. Mwanafunzi atagundua kweli za Biblia ambazo hangeweza kamwe kugundua katika njia nyingine.

2. Mchezo wa kuigiza ni mtindo mzuri sana wa kufundisha. Unaweza kutumiwa kuigiza hadithi za Biblia, na mambo hasa ya maisha.

3. Nji njia moja ya mafunzo inayofurahisha sana.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Chagua tu wanafunzi wanaopenda kushiriki.

2. Hakikisha kwamba mchezo huo unaeleweka kibiblia.

3. Ruhusu mchezo kuendelea tu mpaka kusudi la somo linapofikiwa.

## TARATIBU ZA MCHEZO WA KUIGIZA

1. Tumia vifaa (kama viti, nguo maalum) vichache sana.

2. Usitoe kazi ya kufanya kabla ya wakati.

3. Uache washiriki kusema mistari yao.

4. Soma maandiko kwa ufupi, kisha uchague haraka wale watakaoigiza, kisha muanze.

## MCHEZO

Mchezo unafaa kutumiwa tu wakati wa sherehe kwa sababu wanaoshiriki ni lazima wakariri mistari yao, wawe na vifaa na nguo maalum na wawe na mazoezi mengi. Tumia michezo ya Krismasi, Pasaka au ya siku nyingine maalum.

## MITUNGO

Mtungo ni kama mchezo wa kuigiza katika njia fulani. Ingawaje, kusudi ni tofauti. Mchezo wa kuigiza ni wa kufundisha jinsi watu wanavyojisikia katika hali fulani, lakini mtungo unafundisha juu ya taarifa. Fanya mitungo kama mchezo wa kuigiza, lakini uitumie kueleza somo, kukaza sehemu muhimu au kumaliza somo.

Mitungo ni mizuri sana kutumia wakati unapomfundisha mtu jinsi ya kumshuhudia mwingine. Au, uitumie kufundisha jinsi ya kushauri. Igiza sehemu ile ambayo mtu anakata shauri kuwa Mkristo ili wengine waweze kuona shauri lile analokataa la kumwacha Shetani na kumgeukia Mungu kabisa.

## VIIGIZO VYA KUCHEKESHA

Kiigizo cha kuchekesha ni kama mchezo mdogo ambao mistari yake imekwisha kukaririwa. Tumia kimoja kutangazia tukio fulani muhimu.

Katika ibada kanisani, kijana anaweza kuingia na kujifanya kama anamtafuta rafiki yake. Awaulize watu kadha kama wamemwona. Hatimaye, huyo rafiki asimame na kumwambia, "Yohana, unafanya nini hapa? Unawasumbua watu katika ibada." Naye aseme kwamba amekuja kumtafuta kuhusu mkutano wa vijana. Rafikiye amuulize wakati mkutano huo utafanyika, watakaozungumza na kiini chake.

## UZURI WA VIIGIZO VYA KUCHEKESHA

1. Huwavutia watu.

2. Hufurahisha.

3. Hupasha habari mara moja na kwa nguvu.

## MAMBO YA KUJIHADHARI (MAONYO)

1. Usitumie michezo hiyo kila mara. Itapoteza maana yake.
2. Hakikisha kwamba haichukui dakika tatu au nne.
3. Mwambie mchungaji au kiongozi wa nyimbo mapema ikiwa utatumia kiigizo katika ibada.

## TARATIBU ZA KUTUMIA VIIGIZO VYA KUCHEKESHA

1. Panga mapema kutumia kiigizo cha kuchekesha.
2. Wachague mapema watakaoshiriki katika mchezo huo.
3. Usipayuke-payuke. Nena hasa jambo unalotaka kufundisha.
4. Eleza katika somo sababu iliyokufanya kutumia kiigizo cha kuchekesha. Unganisha somo na mchezo huo.

## MUZIKI (WIMBO)

Mambo mengi yanaweza kufundishwa kwa njia ya muziki (au wimbo). Tumia nyimbo kufundisha historia za Biblia, vitabu vya Biblia, majina ya Mitume au maandiko. Njia nzuri kuhakikisha kwamba wanafunzi walilifahamu somo ni kuwaambia kutunga wimbo juu yake.

## "FLANNELGRAPH"

"Flannelgraph kits" yanaweza kununuliwa au kutengenezwa. Ni vifaa muhimu sana vya kusimulia hadithi. Maagizo ndani yake ni wazi daima. Usitumie "Flannelgraph" mpaka uwe umefanya mazoezi ya kutosha.

Njia hii ni rahisi sana kutumiwa na mwalimu akiwa na ujuzi wake. Mwanzoni inaweza kuonekana kuwa ngumu kwa sababu tarakimu ni lazima kupangwa na kutolewa katika njia inayostahili.

Watoto huvutiwa sana na "Flannelgraph." Rangi zinazong'aa na tarakimu za kuwavutia mara moja.

## MWISHO

Kubadilisha-badilisha njia zako za kufundisha kutakufanya kuwa mwalimu mwema. Jaribu mara kadha. Kutana na waalimu wengine na mfanye mazoezi ya kutumia njia hizi zote. Mnapoendelea kukua, mtagundua ya kwamba kadiri mnavyotumia njia nyingi zaidi ndivyo mnavyofundisha vyema zaidi.

# 8 SASA FUNDISHA

Je, uko tayari kufundisha? Mungu ameiweka nafasi hii ya ajabu mikononi mwako. Jambo lo lote utakalochagua kulifanya ni juu yako.

Usimngojee mtu kuja kwako kukuambia ufundishe. Mungu amekwisha kufanya hivyo. Usingojee ati mpaka waalimu wengine wa kufundisha madarasa mengine wapatikane. Hiyo ni kati ya wale na Mungu. Usingoje ati mpaka uwe hodari wa njia zote zilizoelezwa katika kitabu hiki. Uhodari huo utaupata ukifundisha. Usingoje mpaka umegawanya darasa katika makundi madogo. Mungu atawaita waalimu wengine kukusaidia. Usingoje mpaka upate vifaa vyote vya mafunzo unavyohitaji. Ukiwa na Biblia, unaweza kuanza. Vifaa vinaweza kuagizwa na kupokewa baadaye.

Panga kuanza kufundisha Biblia sasa. Anzisha darasa lako la kwanza katika siku zisizo zaidi ya thelathini. Mungu atakubariki unapoanzisha kazi hii ya kuwafundisha Wakristo.